**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BARAZA LA MITIHANI**

**MTIHANI WA UALIMU DARAJA LA A**

**664** **MITAALA NA UFUNDISHAJI**

**Muda: Saa 3.** **Wednesday, 12th Mei 2010**

---

**Maelekezo.**

1. Karatasi hii ina sehemu **A**, **B** na **C.**
2. Jibu maswali **yote** katika sehemu **A** na maswali **mawili (2)** kutoka sehemu **B** na swali **moja (1)** kutoka sehemu **C**.
3. Sehemu **A** ina alama 36, sehemu **B** ina alama 40 na sehemu **C** ina alama 24.
4. Vifaa vya mawasiliano na vitu vyote visivyoruhusiwa **havitakiwi** ndani ya chumba cha mtihani.
5. Andika **namba yako ya mtihani** katika kila ukurasa wa kijitabu chako cha kujibia.

maktaba.tetea.org
TETEA


Find this and other free resources at: https://maktaba.tetea.org

**SEHEMU A (alama 36)**

Jibu maswali **yote** katika sehemu hii.

1. Eleza maana ya mtaala rasmi.
2. Taja na fafanua kwa ufupi njia tatu (3) ambazo mwanafunzi anaweza kutathminiwa darasani.
3. Kwa nini mtaala unapaswa kuzingatia mahitaji ya wanafunzi?
4. Tofautisha mbinu na mkakati wa kufundishia.
5. Orodhesha vipengele vinne (4) vya andaliola somo vinavyohusiana na utekelezaji wa somo.
6. Fafanua umuhimu wa marejeleo katika andalio la somo.
7. Eleza maana ya Mbinu ya Mradi kama njia ya kufundishia.
8. Taja misingi mitatu (3) ya kisaikolojia inayochukuliwa kama msingi wa mitaala.
9. Kwa nini utabiri wa hali ya hewa huwekwa katika azimio la kazi?

**SEHEMU B (alama 40)**

Jibu maswali **mawili (2)** kutoka sehemu hii.

10. Jadili faida nne (4) ambazo shule na jamii hupata kutokana na ukuzaji bora wa mitaala.
11. Fafanua hatua tano (5) anazoweza kuzitumia mwalimu katika kuandaa na kutoa mtihani mzuri wa mwisho wa muhula.
12. Kwa kutumia somo la Kiswahili au English, andika andalio la somo la dakika 40 kwa kuzingatia hatua zote muhimu.
13. Eleza kwa kina matokeo mabaya yanayoweza kutokea kwa wanafunzi wakati mwalimu hatumii zana za kufundishia ipasavyo.


Find this and other free resources at: https://maktaba.tetea.org

## SEHEMU C (alama 24)

Jibu swali **moja (1)** kutoka sehemu hii.

14. Jadili namna mwalimu anavyoweza kujenga uhusiano mzuri na wanafunzi ili kurahisisha ufundishaji na ujifunzaji.

15. Fafanua jinsi zana za kufundishia zilizotengenezwa na wanafunzi wenyewe zinavyoongeza uelewa wa somo.

16. Eleza umuhimu wa kurekebisha mitaala kwa kuzingatia mabadiliko ya kiteknolojia.


Find this and other free resources at: https://maktaba.tetea.org